**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Ainisha mazoezi manne yanayoweza kukuza stadi ya Kuandika.
2. Bainisha kauli ya utendaji inayowakilishwa katika sentensi ulizopewa.
   (i) Mgala anaimba wimbo kuwa
   (ii) Baba aliitwa shuleni
   (iii) Sentensi Maji yalimwagika ndani
   (iv) Juma na John wanapigana.
3. Chambua kwa ufupi vigezo vinne vitakavyomuongoza kumbaini mshindi katika mashindano ya uandishi wa insha.
4. Thibitisha, kwa kutumia hoja nne, kuwa nahau ni semi zenye umuhimu katika lugha na jamii.
5. Taja mambo manne ya kuzingatia katika mchakato wa kusikiliza hadithi.
6. Bainisha methali zinazowakilishwa na maana alizopewa katika sentensi.
7. Eleza kwa ufupi sifa nne za barua atakayoandika katika gazeti la Mwananchi ili jamii itambue umuhimu wa kuweka mazingira katika hali ya usafi.
8. Eleza kwa ufupi faida nne atakazozipata mwalimu iwapo atatumia kitabu cha ziada kufundishia somo la Kiswahili.
9. Chambua kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika uandishi wa lengo mahsusi.
10. Eleza mambo manne yanayotakiwa kuwepo katika mwongozo wa usahihishaji.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Chambua sifa tano za mtambaji mahiri wa hadithi.
12. Kubali, kwa kutumia hoja tano, kauli isemayo “Kivumishi ni aina mojawapo ya maneno inayojitokeza katika mazingira tofauti tofauti katika sentensi”.
13. Chambua mambo yanayofanyika katika kila hatua ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, yaani katika utangulizi, maarifa mapya, tafakuri na hitimisho.
14. Chambua mambo sita ambayo mwalimu Hamisi anapaswa kuzingatia anapotunga maswali ya insha.